BRELA

WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

ISSN Na: 000401 | Toleo Na 11 | Oktoba-Desemba 2024



BRELA

YAPONGEZWA KUBORESHA HUDUMA KWA NJIA YA MTANDAO

BRELA INAVYOUNGA MKONO JUHUDI ZA SERIKALI .....

WAZIRI JAFO ATOA MSAMAHA WA ASILIMIA HAMSINI



Msajili wa Kampuni anapenda kuwa fahamisha Wadau na Umma kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara ametoa Notisi ya Msamaha wa asilimia hamsini (50%) ya ada ya uwasilishaji wa nyaraka za kampuni nje ya muda iliyotolewa katika Tangazo la Serikali Na. 410 la tarehe 24 Mei, 2024 na itatumika kwa kipindi cha miezi kumi na mbili tangu kuchapishwa kwake.

Waziri ametoa Notisi hiyo kwa kuzingatia kifungu cha 452A cha Sheria ya Kampuni, Sura ya 212 kinachotoa Mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya biashara kutoa msamaha wa ulipaji wa ada ya uwasilishaji wa nyaraka za kampuni nje ya muda. Notisi hii imetolewa kwa lengo la kuwezesha uhuishaji wa taarifa za kampuni zilizosajiliwa kabla ya mwaka 2018 kwenye mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandaoni (Online Registration System - ORS).

Kufuatia notisi hiyo, Msajili wa Kampuni anawataarifu kuwa msamaha wa asilimia hamsini (50%) unatolewa kwa ada ya ucheleweshaji wa nyaraka (late filing fee) kwa Kampuni zenye sifa zifuatazo; Kampuni zilizosajiliwa kabla ya mwaka 2018 ambazo taarifa zake hazijahuishwa kwenye Mfumo wa Usajili wa Kampuni kwa njia ya mtandao; Maombi ya kuhuisha taarifa za kampuni yaliyopo kwenye Mfumo wa usajili wa kampuni kwa njia ya Mtandao, kabla ya tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii; Maombi ya kuhuisha taarifa za kampuni kwenye Mfumo wa Usajili wa Kampuni kwa njia ya Mtandao yatakayopokelewa kwenye mtandao ndani ya muda wa Notisi hii.

Aidha ifahamike kwamba maombi yaliyokwisha wasilishwa kwenye mfumo na kupitishwa na Msajili au Msajili kuingia makubaliano yoyote na Kampuni husika ya jinsi ya kufanya malipo husika kabla ya tarehe ya Notisi hayatahusika na msamaha huu.

Msajili anazielekeza Kampuni zote zinazohusika na msamaha huu kuwasilisha taarifa zao kwa Msajili kupitia mfumo wa ORS ndani ya muda uliolekezwa ili kunufaika na msamaha husika.

YALIYOMO

05



BRELA INAVYOPEPERUSHA BENDERA YA UBORESHAJI WA MAZINGIRA YA BIASHARA

11



BRELA YAPONGEZWA KWA KUBORESHA HUDUMA KWA NJIA YA MTANDAO-MHE. KIGAHE

13



VIJANA 1,500 WA VYUO WAJENGEWA UWEZO NA BRELA

14



ELIMU YAFIKIA WAFANYABIASHARA MBEYA



TAHARIRI

Godfrey Nyaisa

Afisa Mtendaji Mkuu

Heri ya Mwaka mpya 2025. Kama ilivyo ada, ninawakaribisha tena wadau wetu na umma kusoma Toleo letu la Kumi na Moja la Jarida la Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). Toleo hili lina mkusanyiko wa habari na makala mbalimbali zinazoonesha mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Taasisi yetu na ukuaji wa sekta ya biashara hasa katika nyanja ya urasimishaji biashara nchini.

Nafarijika kwamba Taasisi yetu imeuanza mwaka huu, 2025, kwa matumaini makubwa. BRELA itaendelea kutoa huduma bora kwa wadau wetu na umma ili kufikia lengo letu la kuwa Taasisi ya mfano kikanda katika utoaji wa huduma bora za usajili na utoaji wa leseni za biashara.

Katika kipindi hiki, BRELA inafanya jitihada za makusudi za kuboresha utendaji kazi kwa kurekebisha sheria inazozisimamia na kufanya jitihada za makusudi katika kuboresha mifumo ya kiutendaji ili iweze kusomana na mifumo ya taasisi nyingine za Serikali, kurahisisha shughuli za usajili na utoaji wa leseni za biashara. Lengo ni kuunga mkono Serikali ya awamu ya sita na kurahisisha utendaji kazi sambamba na kuwarahisishia wafanyabiashara kupata huduma zaidi ya moja, kwa haraka na kwa muda mfupi.

Katika jitihada hizi BRELA inawafikia wadau wake na umma walio wengi popote walipo. BRELA imekuwa ikitekeleza mkakati wa kutoa elimu kwa umma juu ya upatikanaji wa huduma zake kupitia mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao na jinsi ya kupata huduma hizo kwa urahisi. Katika kujenga mazingira wezeshi kwa maendeleo ya biashara nchini, Taasisi imekuwa ikitoa elimu ya ana kwa ana kwa makundi mbalimbali yakiwemo wanawake na vijana ambao ni wafanyabiashara wapya na wa baadaye.

Pia BRELA imekuwa ikitoa mafunzo mbalimbali kwa wadau wakiwemo wafanyabiashara, na wawekezaji kupitia warsha, semina, pamoja na kushiriki kwenye maonesho mbalimbali yanayowezesha kukutana na wadau ana kwa ana, kuwasikiliza na kutatua kero zao.

Aidha, Taasisi inafanya jitihada za kuhamasisha na kutoa elimu kwa umma kwa kuandaa maudhui yanayotolewa kupitia luninga, redio, magazeti na mitandao ya kijamii ili kujenga uelewa kwa umma.

Ikumbukwe kuwa, urasimishaji wa biashara mara unapokamilika wadau walio wengi wamejijengea dhana kwamba taratibu zimekamilika hapo, la hasha! kuna huduma zingine za kufuata kwa mujibu wa sheria baada ya usajili.

Ili kuhakikisha uhuishaji huo unafanyika, Taasisi imejenga utaratibu, ukaribu na ushirikiano na wadau kwa kutuma ujumbe mfupi wa maneno kwa njia ya simu ili kuwakumbusha wadau wajibu huo kisheria.

Hivyo ninawasihi wadau kutumia fursa hiyo ya ujumbe unaotumwa na Taasisi kuhuisha taarifa zao ili kuepuka kulimbikiza gharama za ada ya ucheleweshaji baada ya usajili.

Nawatakia usomaji mwema wa jarida hili na kukaribisha maoni ya namna ya kuliboresha kupitia simu namba +255 (0) 22 221 2800 au barua pepe yenye anuani maoni@brela.go.tz ili kujenga uhusiano mzuri na jamii na kufikia matarajio yenu.

BODI YA UHARIRI

Andrew Bernad Mkapa - Mwenyekiti

Joyce John Mgaya - Katibu

WAJUMBE

Elieshi Shilekyo Lema

Anabahati Joseph Mlay

Isdory Paul Nkindi

Lameck Samson Nyangi

Stanislaus Aidan Kigosi

Nehemia Mussa Mihayo

BRELA INAVYOPEPERUSHA BENDERA YA UBORESHAJI WA MAZINGIRA YA BIASHARA

Na *Christina Njovu*



Watumishi wa BRELA wakitoa elimu juu ya umuhimu wa kusajili Alama ya Biashara au Huduma kwa washiriki maonesho ya 48 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam (SabaSaba).

Biashara na uwekezaji nchini Tanzania ni sekta zinazotoa fursa nyingi katika kukuza uchumi wa taifa kwa kuwaunganisha wadau wa sekta zinazochangia mnyororo wa uchumi jumuishi, ambao unasaidia kuongeza Pato la Taifa.

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), ni lango kuu la biashara na uwekezaji Tanzania. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1999 imekuwa ikitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria ili kuweka mazingira wezeshi kwa ufanyaji biashara.

Julai 30, 2024 Serikali ilizindua Sera mpya ya Taifa ya Biashara, yenye lengo la kuweka mfumo na mkakati madhubuti wa kuboresha mazingira ya biashara, kuongeza ajira, kuongeza Pato la Taifa, kukuza uchumi, na kuboresha ustawi wa wananchi.

Sera hiyo mpya imeoanisha sera na kanuni za biashara zinazohusiana na masuala ya kibiashara, kuondoa migongano ya kisheria, kuboresha mgawanyo wa majukumu ya kitaasisi, kuimarisha miundombinu ya masoko na biashara, kupunguza muda na gharama z a ufanyaji biashara, kuwezesha biashara mtandao na huduma, usimamizi wa ushindani halali wa kibiashara, na kumlinda mlaji.

Ili kufanikisha lengo hili, BRELA imekuwa ikiboresha mifumo ya kiutendaji inayoiwezesha kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali kwa lengo la kurahisisha usajili na utoaji wa leseni za biashara.

Jitihada hizi zinatokana na tamko la Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kutaka mifumo ya taasisi kusomana, ambapo msisitizo umewekwa kwamba kila kitu kifanyike kwa njia ya mfumo wa kidijitali

Mfumo wa Usajili kwa njia mtandao (Online Registration System - ORS) unaotumiwa na BRELA kutoa huduma umeboreshwa ili kuruhusu mifumo kusomana na taasisi nyingine, hivyo kuwezesha watu kusajili biashara zao mtandaoni bila kulazimika kufika ofisi za BRELA kupata huduma.

Ili kuhakikisha ukuzaji biashara, Serikali imeweka mifumo mizuri ya ufanyaji malipo ya Serikali kwa kutumia namba maalumu ya malipo ili kuziba mianya ya rushwa na kudhibiti urasimu. Hatua hii imerahisisha mazingira kwa wafanyabiashara, hususan wajasiriamali wadogo na wa kati, ili waweze kurasimisha biashara zao na kupata fursa zaidi za masoko ya ndani na nje.

Aidha, urahisishaji wa ufanyaji biashara, mfumo wa Namba ya Utambulisho ya Mlipakodi (TIN) umeunganishwa na usajili wa biashara. Sasa mfanyabiashara hapaswi kwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kupata TIN na kuiwasilisha BRELA; badala yake, namba ya usajili anayopata baada ya kukidhi vigezo vya usajili wa jina la biashara au kampuni ndiyo hutambulika kama TIN yake.

Hali hii imeimarisha ushirikiano kati ya taasisi za Serikali na sekta binafsi ili kuhakikisha huduma zinazotolewa zinakidhi mahitaji ya wafanyabiashara. Kutokana na hilo, BRELA imesaini hati za ushirikiano na taasisi mbalimbali, ikiwemo Tume ya Ushindani (FCC), Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA),



Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), na taasisi za kifedha kama CRDB, NMB, na Exim Bank, ambazo hubadilishana taarifa na BRELA kupitia mfumo wa ORS.

Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2024, utekelezaji wa majukumu ya BRELA ulionesha ongezeko zaidi ya biashara 231,302, zimerasimishwa. Biashara hizi zinaongeza pato la taifa, zinatengeneza ajira za kudumu na za muda mfupi, pia uboreshaji wa miundombinu.

Jumla ya Biashara zilizorasimishwa mwaka 2021 ni 46,360, mwaka 2022 ni 55,294, mwaka 2023 ni 631,179 na mwaka 2024 ni 66,469.

Ongezeko hili linaakisi jitihada za Serikali za kukuza sekta ya biashara kwa kuboresha mifumo ya kielektroniki ya usajili na utoaji wa leseni, sambamba na kutoa elimu kwa umma kuhusu faida za kusajili biashara.

Hatua hii inaonesha ongezeko la ufanisi katika uendeshaji wa taasisi na mashirika ya umma, hasa baada ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kutaka taasisi za umma kuongeza ufanisi na ubunifu.

Hata hivyo, BRELA kupitia Afisa Mtendaji Mkuu wake, Bw. Godfrey Nyaisa, katika mkutano wa wadau wa mwaka 2024, alieleza kuwa BRELA ilifanikiwa kutoa gawio la shilingi bilioni 18.9 kwa Serikali, kama sehemu ya kuunga mkono juhudi za maendeleo ya kiuchumi.

BRELA itaendelea kushirikiana na wadau wake ili kuboresha mifumo ya kiutendaji na kuvutia wafanyabiashara kutoka ndani na nje ya nchi kujifunza kuhusu utoaji wa huduma za mtandao, ikiwemo nchi kama Kenya, Burundi, Sudan Kusini, Korea, na Uganda.

NAIBU WAZIRI MKUU MHE. DKT. BITEKO AIPONGEZA BRELA

Na *Sheila Mfunami*



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Dotto Biteko ameipongeza Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kwa kuendelea kuwafikia wafanyabiashara na kutoa huduma, elimu na hamasa ya kurasimisha biashara zao.

Mhe. Dkt. Biteko ametoa pongezi hizo alipotembelea banda la BRELA na kujionea shughuli za utoaji huduma kwa wananchi wakati wa ufunguzi wa maonesho ya saba ya kitaifa ya teknolojia ya madini yaliyofanyika katika uwanja wa EPZA Bombambili mkoani Geita.

"Endeleeni na kazi nzuri mnayofanya kama taasisi," alisema Mhe. Dkt. Biteko baada ya kushuhudia BRELA ikitoa huduma kwa wananchi wa Geita.

Awali, akitoa maelezo ya lengo la kushiriki maonesho hayo, Afisa Leseni Mwandamizi kutoka BRELA Bw. Koyan Aboubakar, alimweleza Naibu Waziri Mkuu Mhe. Dkt. Biteko kuwa, kama ilivyo dira ya BRELA, hivi sasa ni kuwafikia wadau wengi zaidi pamoja na kutoa huduma za papo kwa papo kwa wananchi.

"Ushiriki wetu katika maonesho kama haya ni kuhakikisha huduma zote za BRELA za usajili wa majina ya biashara, usajili wa kampuni, usajili wa alama za biashara na huduma, utoaji wa hataza, utoaji wa Leseni za biashara kundi "A", usajili wa kiwanda na huduma za kulipia ada za mwaka na uhuishaji wa taarifa za biashara na kampuni zinatolewa papo kwa papo," alisema Bw. Aboubakar.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Busanda, Mhe. Tumaini Brygeson Magessa alipotembelea banda la BRELA aliwataka wajasiriamali wanaoshiriki katika maonesho ya saba ya kitaifa ya teknolojia ya madini kutumia fursa hiyo kurasimisha biashara zao ili zikue.

Mhe. Magessa alionesha pia kuridhishwa na huduma zinazotolewa na kutoa wito kwa taasisi zinazotoa huduma katika maonesho kuhakikisha wajasiriamali wanakua na hivyo kutaka wasaidiwe kwa kupatiwa huduma na elimu ili warasimishe biashara zao.

Aidha, Mhe. Magessa aliipongeza BRELA kwa huduma nzuri za kutoa elimu pamoja na huduma za sajili mbalimbali inazozitoa kwa kuwa zitawawezesha wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa waliojitokeza katika maonesho kupata huduma stahiki za urasimishaji wa biashara zao kwa urahisi.

BRELA ni miongoni mwa taasisi za Serikali ambazo zimeshiriki katika maonesho ya madini kwa lengo la kusogeza huduma kwa jamii hasa kwa kuzingatia kwamba huduma zote zinatolewa kwa njia ya mtandao na zinapatikana papo kwa papo.

Maonesho hayo ya madini yaliongozwa na kaulimbiu isemayo "Matumizi ya Teknolojia sahihi na Nishati safi katika sekta ya Madini kwa maendeleo endelevu".

WAKUFUNZI WAPATIWA MAFUNZO KUHUSU MILIKI BUNIFU

Na Theresa Chilambo



Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kwa kushirikiana na Shirika la Miliki Ubunifu Duniani World Interllectual Property Organization (WIPO) na Shirika la Miliki Bunifu Kanda ya Afrika (ARIPO), pamoja na Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam (UDSM), wameendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wakufunzi watakaokuwa na jukumu la kufundisha wadau mbalimbali juu ya umuhimu na faida ya miliki bunifu ili kuleta chachu ya maendeleo.

Akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo hayo, Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa alisema kuwa maeneo ya Miliki Bunifu ni moja ya changamoto kwa Bara la Afrika, hivyo kwa kushirikiana na wadau wengine BRELA inajumuika kutoa elimu ili kuwajengea uwezo na kuchochea ufanisi katika sekta hiyo yenye utajiri mkubwa.

"Bado kuna changamoto kidogo katika eneo hili la ubunifu kutokana na wadau husika kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu miliki bunifu kutokana na wengi wao kuja na bunifu zao zikiwa hazina sifa, zingine zikitakiwa kurekebishwa ili ziwe na sifa stahiki, kuna nyingine zenye sifa lakini wahusika hawajui namna ya kuzirasimisha," alisema Bw. Nyaisa.

Aidha, kwa kutambua hilo, BRELA wakishirikiana na ARIPO, sambasamba na wadau wengine wameamua kutoa elimu hii ili nao wakafundishe wengine kuhusu Miliki Bunifu; ili kuleta tija stahiki na kuwa chachu kwa maendeleo na kukuza uchumi wa nchi. Aidha Bw. Nyaisa aliongeza kuwa, WIPO ikiwa ndio msimamizi mkuu wa Miliki Bunifu Duniani wameona changamoto ya uwepo wa upungufu wa ufahamu kwa wadau kuhusu masuala ya miliki bunifu, hususani katika nchi za dunia ya tatu. Kupitia mafunzo BRELA itafanya vizuri kupitia miliki bunifu.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam (UDSM), Profesa Willam Anangisye alisema mafunzo hayo ya siku nne yalijikita zaidi katika kuwajengea uwezo Washiriki, kwani dunia ya sasa ni kama kijiji hivyo mafunzo hayo ni muhimu ili wakayatoe kwa wengine na kuleta tija stahiki.

"Kupitia mafunzo haya washiriki wataenda kufundisha wengine namna bora ya kulinda bunifu zao. Kupitia tafiti ambazo zimefanywa inaonesha kuwa watu wengi wamekuwa wakifanya tafiti na kuzifungia kabatini, wakati umefika sasa tafiti hizo ziwe bidhaa kwa ajili ya biashara," alisema Prof. Anangisye.

Naye, Afisa kutoka Wakala



Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam (UDSM), Profesa Willam Anangisye akifungua mafunzo kuhusu miliki bunifu Jijini Dar es Salaam.

wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA), Bw. Mohamed Ali Maalim alisema, mafunzo hayo yatawasaidia kwenda kuwafundisha wabunifu katika maeneo yao ili kujiletea maendeleo, maana miliki bunifu ni mali kama mali nyingine.

"Kupitia elimu hii tutakwenda kuitoa kwa wadau ambao wengi wao hawana elimu ya kutosha ili iweze kuwasaidia kulinda mali zao na kujipatia fedha hivyo kuwa kichocheo kwao kufanya bunifu nyingi zaidi kwa ajili ya kujitengenezea kipato," Alisema Bw. Ali Maalim.

Kwa upande wa Mwakilishi kutoka ARIPO, Bw. Outle Rapuleng, alisema kupitia ushirikiano wao na BRELA pamoja na wadau wengine, wameandaa mafunzo hayo baada ya kuona kuna changamoto ya uelewa mdogo kwa wabunifu kutoka nchi zinazoendelea hususan Afrika.

"Naamini kupitia elimu iliyotolewa itasaidia kupata wakufunzi wengi ambao watakwenda katika maeneo yao na kusambaza elimu kuhusu miliki bunifu hivyo kusaidia kuongeza uwelewa kwa wajasiriamali na kuleta mafanikio yanayotakiwa kupitia tasnia ya miliki bunifu" alisema Rapuleng.

Washiriki wa mafunzo hayo walitoka nchi mbalimbali za Afrika ikiwemo mwenyeji Tanzania, Kenya, Uganda, Malawi, Namibia, Zambia, Botswana na Rwanda.



WAJASIRIAMALI VIJANA WAKUMBUSHWA KURASIMISHA BIASHARA

Na Lungano Mwakyombe





Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imewakumbusha vijana wajasiriamali kurasimisha biashara zao ili kunufaika na soko la ushindani.

Hayo yalisemwa na Afisa Leseni wa BRELA, Bi. Rosemary Otaru wakati akizungumza kwenye hafla ya Panda 2024 iliyoandaliwa na Taasisi ya Her Initiative, Taasisi hiyo ililenga kuwahamasisha na kuwainua wafanyabiashara vijana katika masoko na uboreshaji wa viwanda vya ndani iliyofanyika katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Katika hafla hiyo, Bi. Otaru aliwaeleza wajasiriamali hao umuhimu wa kurasimisha biashara, viwanda pamoja na kupata Leseni ya biashara kundi 'A' ambayo itwawezesha kufanya biashara kitaifa na kimataifa bila usumbufu.

Wajasiriamali vijana wanawake zaidi ya 200, walishiriki ambao wengi wao walishukuru uwepo wa jukwaa hilo kutokana na manufaa waliyoyapata ikiwemo kupata elimu, kupata taarifa za masoko ya bidhaa mbalimbali na kuunganishwa na taasisi pamoja na wadau mbalimbali wa biashara.

Pia walishukuru BRELA kwa namna ambavyo imekuwa ikishiriki na kuwasaidia wajasiriamali kwa kuwapa elimu ya urasimishaji biashara na kuwawezesha kurasimisha biashara zao.

Hafla hiyo ilijikita katika kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika sekta zinazochipukia na ambazo hazipewi kipaumbele hasa viwanda vya urembo vinavyotoa fursa kubwa ya ukuaji na ubunifu kwa wajasiriamali vijana wanawake.

BRELA YAPONGEZWA KWA KUBORESHA HUDUMA KWA NJIA YA MTANDAO-MHE. KIGAHE

Na *Christina Njovu*



Naibu Waziri wa Viwandana Biashara Mhe.ExaudKigahe(Mb) (mwenye miwani katikati), akipata maelezo kutoka kwa Seka Kasera Mkuu wa sehemu ya Miliki Bunifu, juuyautunzajiwaDaftari la Msajili. picha story -mkutano wa Wadau -Naibu Waziri Kigahe

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe (Mb) ameipongeza Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kwa juhudi za kufanya maboresho ya huduma za sajili na utoaji wa leseni za biashara kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa Usajili wa BRELA kwa njia ya Mtandao (ORS) na dirisha la Taifa la biashara (TNBP).

Mhe. Kigahe amebainisha hayo wakati akimwakilisha Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Selemani Jafo katika mkutano wa pili wa BRELA na Wadau wake uliofanyika Oktoba, 2024 Jijini Dar es Salaam ukiwa na lengo la kujadili fursa, mafanikio pamoja na changamoto zilizopo na namna Wakala ilivyojipanga kuhudumia wadau wake siku za mbeleni.

“Matumizi ya mifumo yamepunguza muda, gharama na bughudha kwa wawekezaji na wafanyabiashara ambao walikuwa wanasafiri umbali mrefu kufika katika Ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kupata huduma ”amesema Mhe. Kigahe

Aliongeza kwa kusema kuwa mkutano huu ni muhimu

katika kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya Umma na Sekta Binafsi ili kuweza kujitathimini katika utoaji wa huduma, kupokea maoni ya wadau na kutoa majibu pamoja na kuchukua yale mapungufu kwa ajili ya kuyafanyia kazi, ili kuimarisha ufanisi wa Taasisi katika kuwahudumia wadau wake.

Mhe. Kigahe alieleza kuwa ufanisi wa utendaji kazi wa BRELA ni muhimu katika ujenzi wa uchumi wa nchi yetu kwani ndipo mahali ambapo biashara zinazaliwa na kuanzishwa.

BRELA haiwezi kufanikiwa katika kutekeleza majukumu yake ikiwa peke yake, ni muhimu kushirikiana na kuwa karibu na Sekta za Umma na Sekta Binafsi.

Aidha, Mhe. Kigahe alivutiwa na Kauli Mbiu ya Mkutano huo iliyosema "Mifumo ya Kitaasisi inayosomana na Uwezeshaji wa Biashara Nchini", kwani ina akisi maelekezo ya Serikali kuwa ifikapo mwezi Disemba, 2024 Taasisi ziwe na mifumo inayosomana.

Alitoa rai kwa Taasisi zingine za Serikali ambazo hazina utaratibu wa kuwakutanisha wadau wake kuweza kuiga mfano huo mzuri ili kuweza kujipima kwa kupata maoni na mtazamo kutoka kwa wadau badala ya kujifungia na kujitathmini wenyewe.

Vilevile alisema Serikali imejipambanua kwa uwazi na dhamira ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa kuziwezesha Taasisi za Serikali kutoa miongozo, kuzipa rasilimali fedha, rasilimali watu na vitendea kazi ili watimize wajibu wao kwa ufanisi mkubwa na kufikia malengo ya Serikali. Utoaji wa huduma kwa njia ya mtandao umerahisisha wafanyabiashara kuweza kuomba kusajili au kupata Leseni za biashara wakiwa maeneo mbalimbali na kupata cheti cha usajili au Leseni pale walipo bila kufika katika ofisi za BRELA.

Awali, akimkaribisha Naibu Waziri, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wizara kwa BRELA, Prof. Neema Mori alisema kuwa, Bodi ya Ushauri ya Wizara kwa BRELA itaendelea kusimamia na kutoa ushauri wa jinsi ya kuongeza ufanisi. Hadi sasa bodi imeweza kufanikisha kuongeza mapato ya BRELA na hatimaye kutoa gawio la shilingi bilioni 18 kwa Serikali.

Kwa upande wake, Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa alisema kuwa mkutano umehusisha washiriki kutoka Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekta binafsi, Wawekezaji, Wamiliki wa Viwanda, Wafanyabiashara, Wajasiriamali, Wabunifu, Ofisi za Mawakili na wadau mbalimbali. Uwepo wao utaleta majadiliano yenye tija na manufaa kwa pande zote.



VIJANA 1,500 WA VYUO WAJENGEWA UWEZO NA BRELA

Na *Christina Njovu*





Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imeshiriki kwenye kongamano la kuwajengea uwezo vijana wa vyuo vikuu, kwa kutoa elimu kuhusu urasimishaji wa biashara, ikiwemo usajili wa kampuni, usajili wa majina ya biashara, na usajili wa alama za huduma ili kuhakikisha kuwa biashara zao zinafuata matakwa ya kisheria.

Akitoa mafunzo hayo, Afisa Usajili wa BRELA, Bi. Gift Wazingwa, wakati akiwasilisha mada juu ya umuhimu wa kurasimisha biashara, alieleza kuwa "zipo faida nyingi zinazotokana na kurasimisha biashara zikiwemo utunzaji wa jina la biashara ama kampuni, kupata ulinzi wa kisheria, kuongeza uwezekano wa kupata wabia, kuongeza fursa za upatikanaji masoko pamoja na upatikanaji wa tenda mbalimbali".

Bi. Wazingwa aliongeza kuwa urasimishaji wa biashara unasaidia kuongeza pato la taifa kupitia ada ambazo mfanyabiashara hulipa kwa mwaka, hivyo kuwezesha kutoa huduma mbalimbali za jamii na kuwezesha ujenzi wa miundo mbinu ya kuwafikia wafanyabiashara, ikiwemo ujenzi wa masoko na uwekaji wa mazingira wezeshi ya biashara.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Piga Kitabu Unity ambao ni waandaji wa kongamano hilo, Bw. John Minja amewashukuru BRELA kwa kushiriki na kutoa mafunzo hayo yenye lengo la kumwezesha kijana kutumia uwezo wake kuthubutu na kujiendeleza.

Bw. Minja alisema kuwa ana amini kila kijana ana kitu ambacho amezaliwa nacho, hivyo mafunzo hayo yameongeza ari kutimiza ndoto yake.

Aidha, Bw. Minja ameitaka BRELA kushirikiana kwa karibu ili elimu iliyotoa iwe endelevu na ijulikane kila mahali, kwa kuwa huduma nyingi za kibiashara kubwa ama ndogo zinahitaji huduma za BRELA.

Mwanafunzi wa Chuo cha Afya Morogoro, Bw, Musa Maganza alieleza kuwa, awali alitaka kuanzisha biashara lakini alikosa taarifa sahihi kuhusu taratibu za kuanzisha biashara, hivyo alisema "mafunzo hayo yamenifungua macho na ninatarajia kufungua biashara yangu mkoani Geita" alisema Maganza,

Kongamano hilo lilikutanisha vijana 1,500 kutoka vyuo vikuu na vya kati vilivyopo mkoani Morogoro, vikiwemo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Chuo Kikuu cha Jordan (JUCO) na vyuo vya kati vikiwemo Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Morogoro, Chuo cha Ardhi Morogoro na Chuo cha Afya cha Mtakatifu Malkus Morogoro.

Shirika la Piga Kitabu Unity limekuwa likiandaa makongamano ya aina hii na kutoa mafunzo mbalimbali kuhusu fursa za kujiendeleza kimasomo, mafunzo kwa wanafunzi ambao wanajiandaa kupata ajira na kujiajiri. Kauli mbiu ya kongamano ilikuwa "Chochea maisha yako baada ya kutoka kampasi"

ELIMU YAFIKIA WAFANYABIASHARA MBEYA

Na Lugano Mwakyombe

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imetoa elimu kwa wafanyabiashara pamoja na wamiliki wa kampuni juu ya kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa kwa Msajili wa Makampuni jijini Mbeya.

Elimu hiyo imetolewa na BRELA hivi karibuni ilipoendesha kliniki maalumu kwa wafanyabiashara pamoja na wamiliki wa kampuni jijini Mbeya ili kuwasaidia namna ya kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa.

Afisa Usajili kutoka BRELA, Bw.



Maafisa kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni BRELA wakiwa huduma wafanyabiashara katika kliniki maalumu ya kutoa elimu kuhusu Umuhimu wa Taarifa za UmilikiManufaa.



Grayson Moshi, alisema lengo kuu la kuendesha kliniki hiyo maalumu jijini humo ni kuwahamasisha wadau wa biashara na wamiliki wa kampuni wasiokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa taarifa za Wamiliki Manufaa ili kuwasaidia kuziwasilisha taarifa hizo kwa Msajili wa Makampuni.

Kwa upande wake, Katibu Tawala Msaidizi Idara ya Viwanda, Uwekezaji na Biashara, Bi. Anna Mwambwene wakati akiwakaribisha maafisa wa BRELA ofisini kwake, alisema uwepo wa BRELA jijini Mbeya utasaidia kuwajengea uelewa wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa taarifa za Wamiliki Manufaa na kufanya biashara kisheria.

"Mbeya ni lango la biashara kwa nchi za Jumuiya ya SADC, kwa hiyo wafanyabiashara wengi kutoka Malawi na Zambia wapo hapa mjini hivyo kwa kuendesha kliniki hii kutawasaidia kufanya biashara zao kwa kufuata mifumo inayosimamiwa na BRELA," alisema Bi. Mwambene.

Nao baadhi ya wafanyabiashara ambao walihudumiwa na BRELA katika kliniki hiyo, walionyesha kuvutiwa na utoaji

wa huduma na usaidizi wa kutatua changamoto zao, kama vile kushindwa kuwasilisha taarifa za mwaka za kampuni pamoja na kulipia ada ya utunzaji wa majina ya biashara.

Zaidi ya wafanyabiasara 90 walinufaika na huduma zinazotolewa na BRELA katika kliniki hiyo kwenye maeneo mbalimbali katika Halmashauri za wilaya ya Kyela, Chunya na Mbeya Mjini.

BRELA pia ilitoa mafunzo maalumu ya ukaguzi elimishi kwa wadau wa sekta ya biashara mkoani Dar es Salaam kuhusu Wamiliki Manufaa (Beneficial Ownership) ili waelewe na kuitekeleza kikamilifu.

Mwaka huu Taasisi imejikita katika kutatua changamoto zinazojitokeza wakati wa kufanya sajili mbalimbali na namna kampuni zinavyoweza kuepuka vitendo vya kigaidi, utakatishaji fedha haramu na kukwepa kodi.

Ukaguzi elimishi uliofanyika katika Mkoa wa Dar es Salaam hivi karibuni kwa wafanyabiashara uliambatana na utoaji wa huduma za papo kwa papo za sajili mbalimbali za huduma zinazo tolewa na BRELA.

USAJILI WA MILIKI BUNIFU HUONGEZA THAMANI YA BIDHAA

Na *Stanislaus Kigosi*



Mvumbuzi wa taa za vifuu vya nazi (coconut lamp) na vyombo vya mbao Bw. Ditrick Mbena akionesha ubunifu wa bidhaa zake kwenye maonesho ya kimataifa ya biashara (Saba saba), Dar es Salaam

Miliki bunifu kama zilivyo mali nyingine zinazoshikika, pindi inapokuwa imerasimishwa na kupata ulinzi wa kisheria ndivyo thamani yake inavyo ongezeka. Hii ni kama nyumba inayokuwa imejengwa katika kiwanja ambacho hakina hatimiliki; hata ingekuwa imejengwa kwa gharama kubwa, thamani yake haiwezi kuwa sawa na nyumba ya kawaida iliyojengwa kwenye kiwanja kilichorasimishwa kwa kupewa hatimiliki. Kadhalika, kazi ya miliki Ubunifu ambayo haijasajiliwa, thamani yake ni ndogo hata kama imeundwa kwa ubunifu mkubwa na wenye kuvutia sana.

Sheria zinazosimamia ulinzi wa Miliki Ubunifu kama vile Hakimiliki au Miliki Ubunifu zinazohusu uzalishaji wa viwandani hazilazimishi wamiliki kuzisajili ili zilindwe.

Sheria zote zimetoa hiyari kwa wamiliki kusajili ama kutokusajili, lakini kutokusajili mali zote zitokanazo na miliki ubunifu inaweza kusababisha wamiliki kupoteza haki zao ambazo zipo katika miliki ubunifu pindi inapotokea migogoro ya umiliki au inapotokea uharamia umefanyika katika kazi za miliki ubunifu.

Kusajili Miliki Ubunifu kunatoa ulinzi kwa wamiliki, lakini pia huongeza thamani ya miliki ubunifu hivyo kuwafanya wamiliki kuweza kutumia ubunifu huo kuwazuia wengine kutumia miliki ubunifu bila ridhaa ya mwenye nayo. Ridhaa hiyo inaweza kuwa ni kwa kuuziwa au kukodishiwa ili mtu mwingine aitumie kwa wakati fulani kwa malipo maalumu kama ambavyo wanaweza kukubaliana.

Usajili wa alama za biashara na huduma, mathalani humpatia mmiliki wa biashara na huduma husika nafasi ya kuitofautisha biashara au huduma yake na zile zinazotolewa na washindani wake. Pamoja na hayo, huwazuwia washindani wake kuiga alama yake ya biashara au huduma kwa

kuiweka katika bidhaa au huduma wanazozitoa katika soko.

Wafanyabiashara hutumia nguvu na gharama kubwa sana kufikisha bidhaa na huduma zao kwenye masoko, pia kujenga uaminifu kwa wateja wao. Mara zote hutumia alama zao za biashara kutangaza bidhaa na huduma wanazozalisha.

Hivyo, inaweza kutokea mfanyabiashara mmoja akatumia nguvu na gharama kubwa kujijenga kwenye soko kwa kutumia alama yake ya biashara, lakini kama hiyo alama yake ya biashara haijasajiliwa, anaweza kukuta mshindani kibiashara ama ameamua kuisajili alama hiyo na hivyo kumfanya yeye asiweze kuitumia tena.

Sambamba na hilo, katika mazingira sawa na hayo, anaweza kutokea mfanyabiashara mwingine au mshindani katika biashara akaamua kughushi au kuitumia alama hiyo ya biashara kwa kutoa bidhaa au huduma duni tofauti na zile ambazo zinatolewa na mmiliki halisi wa alama ya biashara au huduma. Kitakachotokea katika mazingira hayo, ni kuvunja uaminifu ambao mmiliki wa alama ya biashara husika alishapata kutoka kwa walaji wa bidhaa na huduma zake. Hali hii ikitokea inaua biashara ya yule ambaye ni mmiliki halisi wa alama hiyo ya biashara na hivyo kuathiri mfumo wa biashara, ushindani wa kibiashara na uchumi wa nchi nzima.

Sheria za Miliki Ubunifu huwatambua na kuwalinda wale ambao wamefanya usajili wa mali zao za miliki ubunifu na kuwalinda dhidi ya wengine ambao hawajafanya usajili.

Katika mazingira ya ushindani wa biashara, wafanya biashara ni vema kuwa makini kwa kuhakikisha kuwa wanazilinda alama zao za biashara kwa kuzisajili kwenye Ofisi ya Msajili wa Alama za Biashara ambayo kwa hapa Tanzania Bara, Ofisi ya Msajili ni Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). Hii ndiyo ofisi inayotoa ulinzi wa alama za biashara na huduma kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Namba 12 ya mwaka 1986.

Hali kadhalika, kuhusu ulinzi wa uvumbunzi ambao hulindwa na Sheria ya Hataza, mvumbuzi yeyote kabla hajauweka hadharani uvumbuzi wake inampasa kwanza aanze utaratibu wa kusajili ulinzi wa hataza yake ndipo aweke hadharani uvumbuzi huo.

Uvumbuzi ndiyo chachu ya maendeleo ya teknolojia ambayo hutumika katika uzalishaji wa bidhaa viwandani, hutumika katika kutoa huduma za afya kwa kuvumbua vifaa tiba pamoja na dawa za matibabu na chanjo za maradhi mbalimbali.

Mvumbuzi anapoacha kusajili uvumbuzi wake kwenye Ofisi ya Msajili wa Hataza ambayo kwa hapa Tanzania ni BRELA, uvumbuzi wake unaweza kuibwa na watu wengine ambao wanaweza kuutumia uvumbuzi huo kujinufaisha wao wenyewe kiuchumi bila mvumbuzi kunufaika kwa lolote.

Ifahamike pia kuwa uvumbuzi ukishasajiliwa na kupata cheti cha hataza unaweza kuuzwa kwa wazalishaji ambao wao wanaweza kuuzalisha kwa wingi au kuitumia teknolojia hiyo kuzalisha zaidi na kumpa mbunifu binafsi faida za kiuchumi na kuongeza tija na kipato kwa nchi.



A TO Z: MAHITAJI YA KUOMBA LESENI YA BIASHARA KUNDI ‘A’

Na Sweetness Madata

Maendeleo ya nchi yoyote yanategemea kwa kiasi kikubwa maendeleo ya sayansi na teknolojia, ambayo yameleta utatuzi wa changamoto mbalimbali duniani.

Hali hii imewezesha pia maendeleo ya uchumi nchini Tanzania, hususan katika sekta ya viwanda na biashara.

Mazingira ya biashara nchini yameboreshwa kwa uwepo wa mifumo mbalimbali ya urasimishaji biashara chini ya usimamizi wa wizara na taasisi za Serikali.

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), ni moja ya taasisi nchini inayotoa huduma zake zote kwa njia ya mtandao, ikiwezesha wafanyabiashara na wadau duniani kote kuzipata huduma hizi kwa urahisi.

Makala hii itakujuza kuhusu mahitaji muhimu ya kuzingatia ili kutumia fursa ya kupata Leseni ya Biashara Kundi ‘A’ kwa njia ya mtandao ukiwa popote pale ndani na nje ya nchi.

Leseni ya biashara ni cheti kinachotolewa na Serikali kwa mfanyabiashara kwa ajili ya kumruhusu kufanya biashara nchini. Leseni za biashara zimegawanywa katika makundi mawili: Kundi ‘A’ na Kundi ‘B’.

Leseni za biashara Kundi ‘A’ hutolewa na BRELA kwa biashara zenye sura ya kitaifa au kimataifa, zinazohusiana na maamuzi ya kisera katika



Afisa Leseni kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA Bi. Sweetnes Madataa kimkabidhi cheti cha usajili mdauwa BRELA baada ya kukamilisha mchakato wa kurasimi shabiashara yake.

ngazi ya kitaifa au kimataifa.

Mfano wa biashara zinazohitaji Leseni hizi ni uingizaji wa bidhaa kutoka nje (import), Usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi (export), huduma za kifedha kama benki na taasisi za mikopo midogo, pamoja na usafirishaji wa abiria na bidhaa ndani na nje ya nchi.

Endapo mwombaji atakamilisha vigezo vyote, anaweza kupata leseni yake ndani ya siku tatu za kazi, kulingana na Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa BRELA (vingine vikienda sawa).

Leseni za biashara Kundi 'B' hutolewa na mamlaka za Serikali za mitaa kwa biashara zisizo na sura ya kitaifa au kimataifa. Mfano wa biashara hizi ni gereji, saluni, ujenzi, ushauri wa kitaalamu, maduka ya rejareja na jumla, na nyinginezo.

Kwa lengo la kusogeza huduma karibu, Serikali ilitengeneza mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama "Dirisha la Taifa la Biashara" (TNBP) ili kutoa taarifa za kibiashara na leseni kwa njia ya mtandao.

Mfumo huo ndiyo unatumika kutoa Leseni za Biashara Kundi 'A' kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya www.business.go.tz.

Ili kuomba Leseni ya Biashara, mwombaji anatakiwa kuwa na barua pepe inayofanya kazi na namba ya simu kwa ajili ya usajili.

Baada ya usajili, atapewa jina la mtumiaji na neno la siri kwa ajili ya kuingia katika mfumo. Ombi la leseni hufanywa kwa kujaza fomu mtandaoni na kuambatisha nyaraka muhimu.

Nyaraka hizo ni pamoja na Hati ya usajili wa jina la biashara au kampuni, Katiba ya kampuni au dondoo kutoka kwa msajili, Uthibitisho wa uraia wa mmiliki/wamiliki wa biashara au kampuni (cheti cha kuzaliwa, Kitambulisho cha Taifa, Kadi ya mpiga kura, au Pasi ya kusafiria).

Nyaraka nyingine ni uthibitisho wa mahali pa kufanyia biashara (mkataba wa pango au hati ya umiliki), Hati ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN), pamoja na kibali kutoka kwa mamlaka ya udhibiti kulingana na aina ya biashara, mfano TCRA, TBS, TRA.

Mfumo wa TNBP umeunganishwa na Mfumo wa Malipo ya Serikali (GePG), hivyo kurahisisha malipo ya ada za leseni kulingana na aina ya biashara.

Matumizi ya mfumo huu yameleta faida mbalimbali kwa wafanyabiashara na Serikali, zikiwemo: kupunguza haja ya kufika BRELA kwa ajili ya kuwasilisha maombi ya leseni, kuongeza ufanisi kwa kupunguza muda wa utoaji wa leseni hadi siku tatu za kazi, na kuwezesha utunzaji mzuri wa taarifa za leseni kwa ajili ya takwimu sahihi za sekta ya biashara na viwanda.

Ni muhimu sana kwa kila mfanyabiashara kujua kuwa Leseni za biashara ni nyenzo muhimu ya kisheria kwa ajili ya kusimamia biashara nchini. Kumiliki leseni ni hatua muhimu inayothibitisha kuwa biashara inayofanyika inazingatia sheria.

Wafanyabiashara wanahimizwa kuzifahamu na kuzitii sheria za nchi, ikiwa ni pamoja na Sheria ya Leseni za Biashara na sheria nyingine zinazohusiana na biashara.



Ikiwa bado hujapata Leseni yako ya Biashara Kundi 'A', tembelea ***www.business.go.tz*** kwa ajili ya kupata huduma hii aukwa maelezo naufafanuzi zaidi, ***pigasimunamba +255 222 212 800.***

USAJILI NA UTOAJI WA VYETI VYA USAJILI NA LESENI

Na *Rosemary S, Otaru*



Viwanda ni moja ya sekta muhimu katika kutengeneza ajira na kuchangia Pato la Taifa.
Hapa nchini, viwanda vinasajiliwa na kupatiwa aidha Cheti cha Usajili au Leseni ya Kiwanda kutegemea na kiwango cha mtaji wa kiwanda husika.

Ili kuelewa dhana ya usajili na utoaji wa leseni za viwanda ni vyema tukaelewa sheria inayosimamia usajili na utoaji wa leseni za viwanda.

Sheria ya Leseni na Usajili wa Viwanda ya Taifa, Sura ya 46 inasimamia na kuratibu usajili na utoaji wa Vyeti vya Usajili/ Leseni za Viwanda kwa pande zote mbili za Muungano (Tanzania Bara na Zanzibar).
Sheria hii ilianza kutumika baada ya kusainiwa na Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius K. Nyerere tarehe 27 Aprili, 1967 ikilenga kuwezesha uendelezaji wa viwanda kwa njia ya kuvisajili na kuvipa Vyeti vya Usajili/ Leseni za Viwanda.

Kwa upande wa Tanzania Bara, sheria hiyo inasimamiwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kwa upande wa Zanzibar sheria hii inasimamiwa na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda.

Kiwanda ni sehemu au mahali popote ambako shughuli za uzalishaji zinafanyika na shughuli hizo za uzalishaji zinaweza kutumia mikono au mashine, zinazohusisha ubadilishaji wa malighafi kuwa bidhaa kwa ajili ya kutumika na mtumiaji wa mwisho au kutumika kama malighafi kwenye kiwanda kingine kama ilivyoelezwa kwenye Kifungu cha 2(a) cha sheria tajwa.

Kwa sasa, pamoja na huduma zingine zinazotolewa na wakala (BRELA), usajili na utoaji wa leseni za viwanda hufanywa kwa njia ya kielektroniki kupitia Mfumo wa Usajili Kwa njia ya Mtandao (ORS), ikihusisha uwasilishaji wa maombi, kufanya malipo, kuchakata maombi na kupokea Cheti cha Usajili/ Leseni ya Kiwanda husika.

Cheti cha Usajili (*Certificate of Registration*) hutolewa kwa kiwanda kidogo chenye mtaji usiozidi Shilingi za Kitanzania milioni 100, wakati Leseni ya Kiwanda (*Industrial Licence*) hutolewa kwa kiwanda chenye mtaji wa zaidi ya Shilingi za Kitanzania milioni 100 kama ilivyoelezwa kwenye Kifungu cha 5, 9 cha sheria tajwa hapo juu, ikisomwa pamoja na Kanuni ya 8 ya sheria hiyo.

Mwombaji wa Cheti cha Usajili/ Leseni ya Kiwanda anapaswa kuwa amesajili Kampuni au Jina la Biashara au taasisi nyingine yeyote kama vile Taasisi zisizo za Serikali (NGO) n.k, na kisha kupitia Mfumo wa ORS (www.brela.go.tz) atajaza taarifa kamili za kiwanda husika na kupakua (*Download*) kutoka kwenye mfumo huo Fomu ya Maombi (*Consolidated form*) yenye taarifa alizojaza, kwa

ajili ya kusainiwa na kupakia (*Upload*) kwenye mfumo huo, ikiwa imeambatishwa na mchanganuo wa mradi, nyaraka yeyote inayothibitisha kuwa eneo kilipo kiwanda ni kwa matumizi ya viwanda kama vile Hati ya kiwanja au Mkataba wa pango au barua kutoka kwa Mamlaka ya Mipango Miji ya Halmashauri husika pamoja na kufanya malipo ya ada ya ombi husika.

Cheti cha Usajili/Leseni ya Kiwanda hutolewa ikiwa na masharti mbalimbali kulingana na aina ya bidhaa inayozalishwa ndani ya siku moja (1) mpaka tatu (3) kwa maombi yaliyokidhi vigezo.

Wakala inatoa wito kwa wamiliki wote wa viwanda kurasimisha viwanda vyao kwakuwa ni hatua muhimu kwa mustakabali wa sekta ya viwanda na taifa kwa ujumla.

Kwa upande wa Wamiliki wa Viwanda, usajili na utoaji wa Leseni za Viwanda, ni hatua muhimu katika urasimishaji wa biashara ambako kupitia usajili huo, viwanda husika vinaweza kunufaika na fursa mbalimbali kama vile kupata mitaji kutoka katika taasisi za kifedha, kutanua wigo wa masoko na kutambulika na taasisi/ mamlaka nyingine za kiserikali pamoja na sekta binafsi.

Kwa upande wa Serikali, usajili na utoaji wa Leseni za Viwanda, unaisaidia kupata takwimu sahihi za idadi, aina na uwezo wa viwanda vilivyopo, ajira, aina ya bidhaa, kiasi kinachozalishwa, malighafi inayotumika, na michango mingine katika uchumi wa taifa kama vile kuwezesha ushindani sawa sokoni, kuongeza mapato, na kusaidia kuweka sera na mipango mbalimbali kwa manufaa ya sekta ya viwanda na taifa kwa ujumla.



MUUNGANO WA MIFUMO : CHACHU YA MABADILIKO KWA WAJASIRIAMALI WANAWAKE TANZANIA

Na Mwandishi Wetu



Katika enzi ya kidijitali, mifumo bora na iliyounganishwa ina jukumu muhimu katika kuunda mazingira bora ya biashara.

Kwa wajasiriamali wanawake nchini Tanzania, kusomana kwa mifumo ya kitaasisi unaashiria mabadiliko makubwa kwa jinsi biashara zinavyoanzishwa, kusimamiwa na kukuzwa.

Muunganiko ulioboreshwa wa mifumo mbalimbali ya Serikali na sekta binafsi unabadilisha mandhari na kuwawezesha wanawake kuondokana na vikwazo na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Maendeleo haya yana uwezo wa kukuza sio tu ujumuishaji zaidi, lakini pia kukuza ukuaji katika tasnia ya biashara.

Makala haya yanachunguza njia kuu za muingiliano kubadilisha mfumo wa biashara kwa wanawake kote Tanzania ambao kijadi wamekabiliana na vikwazo vingi zaidi katika kupata rasilimali, usaidizi, mitandao na jinsi wanavyoingiliana na mfumo.

Hapo awali, kumekuwa na changamoto zaidi kwa wanawake wanaoanzisha biashara wale wa maeneo ya vijijini, imekuwa ni mchakato mrefu na mgumu wa usajili.

Katika kusajili biashara ilihitaji hatua nyingi na mashirika mengi, kila moja ikiwa na seti yake ya fomu, ratiba na ada.

Kwa hivyo, wanawake walipata changamoto kukabiliana na mfumo huo kutokana na vikwazo vya muda, ukosefu wa rasilimali, au upatikanaji mdogo wa taarifa.

Hali ya kugawanyika kwa mifumo ya biashara ilimaanisha kuwa wanawake, hasa wale walio katika sekta zisizo rasmi, mara nyingi walibaki nyuma na kutoonekana katika uchumi rasmi. Kutoonekana huku kulizuia ufikiaji wao kwa ulinzi wa kisheria, manufaa ya usalama wa jamii na huduma zingine muhimu. Muingiliano wa Mfumo huhakikisha kuwa biashara inaposajiliwa inatambuliwa katika mifumo tofauti.

Utambuzi huo huwapatia wanawake utambulisho wa kisheria kama wajasiriamali lakini pia huwafanya wastahili usaidizi wa Serikali, kama vile ruzuku, au programu za mafunzo.

Ujio wa kusomana kwa Mfumo wa Usajili wa BRELA kwa njia ya Mtandao (ORS) na mifumo ya taasisi nyingine za Serikali ambayo inasimamiwa na NIDA, TRA, PPRA, imewawezesha wanawake kukamilisha usajili wa biashara kwa haraka na kwa ufanisi zaidi kwa mfano; mwanamke mjasiriamali anapoomba usajili wa biashara, mfumo huthibitisha moja kwa moja kitambulisho chake cha Taifa na NIDA na usajili wa kodi na TRA, hivyo kupunguza hitaji la kutembelea ofisi mbalimbali. Hii imepunguza muda wa kusajili biashara kutoka kwa wiki hadi siku chache tu, na kuondoa kikwazo kwa wanawake.

Ushirikiano hupunguza hitaji la wanawake kujihusisha na ofisi nyingi, kazi ambayo hapo awali ilihitaji wakati na rasilimali za kifedha. Sasa, kupitia mifumo iliyounganishwa, wanawake wanaweza kupata huduma mtandaoni au kupitia vituo ndani ya kituo kimoja, na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa vikwazo hivi visivyo rasmi.

Ushirikiano zaidi unaziba pengo kati ya taasisi za Serikali na watoa huduma za kifedha. Ushirikishwaji katika mifumo ya kifedha bado ni changamoto kubwa kwa wanawake wengi nchini Tanzania, kwani asilimia ndogo tu ndiyo wanaopata huduma rasmi za kibenki.

Kwa kuunganisha BRELA na taasisi kama TRA na taasisi za fedha , wanawake wajasiriamali sasa wanaweza kupata huduma za kifedha kwa urahisi zaidi, ikiwa ni pamoja na mikopo, akaunti za akiba na suluhu za malipo ya kidijitali. Matokeo yake, ushirikiano huwapa wanawake zana za kifedha zinazohitajika kupanua biashara zao na kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya kiuchumi.

Mabadiliko ya kuelekea mifumo inayoweza kushirikiana yameleta msukumo mpana wa kusoma na kuandika kidijitali na ubunifu. Kwa vile mifumo hii inahitaji biashara kuingiliana mtandaoni, wajasiriamali wengi wanawake wamechukua fursa hiyo kujenga ujuzi wa kidijitali, na kuongeza uwezo wao wa jumla wa kustawi katika mazingira ya kisasa ya biashara yanayoendeshwa na teknolojia.

Mipango ya Serikali, kwa ushirikiano na washirika wa sekta binafsi, inatoa programu za mafunzo kwa wanawake katika zana za kidijitali, mifumo ya biashara ya mtandaoni na ujuzi wa kifedha, ambayo yote ni muhimu kwa ulimwengu unaozidi kuunganishwa. Kadhalika, ushirikiano umerahisisha wanawake kupata masoko zaidi ya maeneo yao ya biashara.

Kwa mifumo ya kidijitali iliyounganishwa na mifumo ya fedha, biashara na forodha, wanawake sasa wanaweza kupanua biashara zao katika masoko ya kikanda au kimataifa bila michakato migumu, ambayo hapo awali, ilifanya biashara isiweze kufikiwa na biashara ndogo ndogo.

Muunganiko usio na mnyororo wa mifumo sio tu huwanufaisha wajasiriamali wanawake, bali pia huchangia ukuaji na ushirikishwaji wa uchumi wa Tanzania. Kulingana na tafiti, wanawake wanapowezeshwa kiuchumi, huwekeza zaidi katika familia na jamii zao, na hivyo kusababisha athari ya kuzidisha ambayo huongeza ustawi wa kijamii kwa ujumla.

Msukumo wa Serikali ya Tanzania kuelekea kwenye mfumo wa kidijitali na muingiliano wa mifumo pia unawiana kwa karibu na mipango mipana inayolenga kufikia usawa wa kijinsia na maendeleo endelevu; kuwawezesha wanawake kurasimisha biashara zao, kupata rasilimali za kifedha na kupunguza muda na juhudi zinazohitajika. Ili kuzingatia mahitaji ya udhibiti, Serikali inaweka msingi wa uchumi shirikishi zaidi ambapo wanawake wanaweza kustawi pamoja na wanaume.

Wakati Tanzania inaendelea kuweka mkazo katika matumizi ya mifumo iliyounganishwa kidijitali, wanawake wanasimama kuwa miongoni mwa wanufaika wakubwa, kupata zana, rasilimali, na imani i nayohitajika ili kufanikiwa katika mazingira ya biashara yenye ushindani. Hili si jambo la kubadilisha kwa wanawake; ni chachu ya maendeleo ya jumla ya nchi na ukuaji wa uchumi.

BRELA YATAKIWA KUENDELEZA USHIRIKIANO NA WADAU WAKE

Na Gerard Nyang!ali





Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imetakiwa kuendelea kushirikiana na wadau wake katika masuala mbalimbali ya kiteknolojia kwa lengo la kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini na kuondoa changamoto.

Wito huo umetolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara Mhe. Balozi Dkt. John Simbachawene wakati wa maadhimisho ya miaka 10 ya SCANCODE iliyofanyika katika ukumbi wa ofisi za COSTECH jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Katika hotuba yake ya ufunguzi wa maadhimisho hayo, Mhe. Dkt. Balozi Simbachawene alisema ni muhimu Taasisi za Serikali zinazohusika na masuala ya viwanda na biashara kama vile BRELA ziendeleze mashirikiano na SCANCODE ili kuwasadia wafanyabiashara na wajasiriamali kuondokakana na bidhaa bandia sokoni.

Akizungumzia namna ambavyo BRELA inavyotekeleza majukumu yake, Afisa Sheria kutoka taasisi hiyo Bi. Vicencia Fuko alisema, kwa sasa Wakala imefanikiwa kukabiliana na vishoka kwani shughuli zote zinafanyika kwa njia ya mtandao ORS na kuwanyima fursa ya kuwalaghai na kuwaliza wateja.

“BRELA ni moja ya Taasisi ya Serikali ambayo inasimamia sheria, hasa zinazohusika na uendeshaji wa biashara nchini pamoja na kutoa leseni za biashara ambao kwa sasa huduma zote zimerahisishwa na zinapatikana kwa njia ya mtandao wa ORS” alsema Bi. Fuko.

Aidha, Bi. Fuko aliwataka wadau wa BRELA kutosita kuwasiliana na Wakala kupitia Kituo cha Miito (Huduma kwa Wateja) pale wanapopata changamoto au hata kufika katika Ofisi za BRELA zilizopo mtaa wa Shaban Robert, Posta jijini Dar es Salaam.

BRELA pia ilitumia maadhimisho ya miaka 10 ya SCANCODE kutoa mafunzo na elimu ya urasimishaji biashara kwa washiriki ambao wengi ni wajasiriamali na baadhi ya Taasisi zilizohudhuria maadhimisho hayo.

SCANCODE ni kampuni bunifu ya teknolojia ya mawasiliano (ICT) ambayo imeanzishwa na kijana wa Kitanzania na kusajiliwa katika Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni BRELA huku ikipatiwa uhakiki na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) kwa njia hatamizi.

Kampuni ya SCANCODE ilianzishwa mwaka 2014 na imekuwa ikifanya kazi za kuwasaidia wajasiriamali hasa wazalishaji kupambana na bidhaa feki sokoni kwa kutumia Msimbo Milia (Barcode) ambayo hubandikwa kwenye bidhaa kabla haijafikishwa

UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA KAMPUNI BAADA YA USAJILI

Msajili wa kampuni anapenda kuwataarifu Wamiliki, Wakurugenzi na Makatibu wa makampuni kwamba baadhi ya makampuni yamekuwa hayatekelezi wajibu wao wa kisheria wa kuwasilisha kwa Msajili wa Makampuni Taarifa za Mwaka na Mizania (**Annual Returns and Audited Accounts**) za Kampuni kama Sheria ilivyoelekeza.

Sheria pia, inayataka Makampuni ya Kigeni (**Foreign Companies**) kuwasilisha Mahesabu yake ya Mwaka kila mwisho wa mwaka (**Calendar Year**).

Taarifa hizi zinatakiwa kuwasilishwa kwa Msajili wa Makampuni kila ifikapo tarehe na mwezi ambao kampuni ilisajiliwa (**anniversary of incorporation**) au tarehe nyingine yoyote ambayo Kampuni itakuwa imeichagua na kumtaarifu Msajili wa Makampuni nae akaridhia. Sharti hili ni kwa mujibu wa Kifungu cha 128 cha Sheria ya Makampuni, Sura 212.

Msajili wa Makampuni anapenda kuwafahamisha na kuwakumbusha kwamba, kuanzia sasa, Taarifa za Mabadiliko yoyote yanayoletwa na kampuni hayatafanyiwa kazi mpaka Kampuni husika itakapokuwa imewasilisha Taarifa zake za Mwaka.

Taarifa za Mwaka na Mahesabu ya Mwaka kwa kampuni za kigeni (**Foreign Companies**) husaidia kutoa taswira halisi ya Kampuni, hivyo humuwezesha Msajili wa Makampuni kuwa na taarifa sahihi za Kampuni husika. Makampuni yanahimizwa kuwasilisha Taarifa za Mwaka ili kuepuka usumbufu unaoweza kutokea wakati kampuni inawasilisha taarifa za mabadiliko mbalimbali yanayotokea katika kampuni.

Tembelea www.brela.go.tz

ili kupata huduma hii

@brela_tanzania @brela_tanzania @brela_tanzania brelaonlinetv



JENGO LA BRELA

Kitalu Na 20,

Kiwanja Na 23 Sokoine,

Drive/Mtaa wa Shaaban Robert

P.O. Box 9393, 11101 Dar es Salaam

Simu: +255 222 212 800,

Barua Pepe: ceo@brela.go.tz

usajili@brela.go.tz

Tovuti: www.brela.go.tz

@brela_tanzania

@brela_tanzania

@brela_tanzania

www.brela.go.tz

eMrejesho

*150*00#

CHAGUA 9, KISHA 2

Pakuwa eMrejesho kwenye

GET IT ON Google Play